**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MWALIKO WA TAASISI, ASASI ZA KIRAIA ZENYE NIA YA KUTOA ELIMU YA MPIGA KURA NA UANGALIZI WAKATI WA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI WA MWAKA 2025

Dar es Salaam, 19 Aprili, 2025.

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake cha tarehe 03 Aprili, 2025, imetoa mwaliko kwa taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura na uangalizi wakati wa uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani wa Mwaka 2025. Maombi yatapokelewa kuanzia tarehe 21 Aprili, 2025 hadi 20 Mei, 2025.

Tume imetoa mwaliko huo kwa kuzingatia kifungu cha 10(1)(g) na (h) cha Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024, kinachoipa Tume jukumu la kutoa elimu ya mpiga kura nchini, kuratibu na kusimamia taasisi na asasi zinazotoa elimu hiyo. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 85(4) cha Sheria Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya Mwaka 2024 na kanuni ya 13(1) na (2) ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, Tume hutoa mwaliko kwa taasisi na asasi za ndani na za kimataifa zinazokusudia kushiriki katika zoezi la uangalizi wa uchaguzi.

Taasisi na asasi za kiraia zenye nia ya kutoa elimu ya mpiga kura zinatakiwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa katika Mwongozo wa Elimu ya Mpiga Kura wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ambavyo ni: -

(i) iwe imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania;

(ii) iwe imefanya kazi nchini kwa kipindi kisichopungua miezi sita tangu kusajiliwa kwake;

(iii) ikiwa taasisi au asasi ya kiraia inahusisha watendaji wa kimataifa, miongoni mwa watendaji wake wakuu watatu, wawili wawe Watanzania;

(iv) katika utendaji wake, iwe haijahusishwa na uchochezi au kuvuruga amani;

(v) iwe na uzoefu wa kutoa elimu ya mpiga kura; na

(vi) iwe tayari kujigharamia katika kutoa elimu ya mpiga kura.

Aidha, waombaji wa uangalizi wa uchaguzi wanatakiwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa kwenye Mwongozo wa Waangalizi wa Uchaguzi wa Mwaka 2025 ambayo yanawataka kuanisha: -

(i) anuani ya taasisi au asasi husika;

(ii) mahali ambapo taasisi au asasi husika inafanyia kazi;

(iii) shughuli ambazo zinafanywa na taasisi au asasi husika kwa mujibu wa hati ya usajili;

(iv) sehemu ambazo taasisi au asasi inapenda kwenda kuangalia uchaguzi;

(v) idadi ya watu ambao taasisi au asasi itawatumia katika zoezi hilo pamoja na majina na taarifa zao binafsi;

(vi) majina na namba za simu za viongozi wa taasisi au asasi husika;

(vii) ikiwa taasisi au asasi ya ndani inahusisha viongozi ambao si raia wa Tanzania, viongozi wawili ni lazima wawe watanzania;

(viii) kuambatisha nakala au kivuli cha hati au nyaraka ya usajili wa taasisi au asasi husika; na

(ix) kuambatisha nakala au kivuli cha katiba ya taasisi au asasi husika.

Maombi yanapaswa kufanyika kupitia kupitia kiunganishi (link) **https://ams.inec.go.tz** katika Mfumo wa Kusajili Watazamaji, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari (Accreditation Management System - AMS). Aidha, maombi yatakayotumwa kwa njia tofauti na mfumo ulioainishwa hayatafanyiwa kazi.

Imetolewa na:

Kailima, R. K
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**